MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
VETA NKASI

Simu : 255 - 736117116
Barua-pepe: nkasidvtc@veta.go.tz

Mkuu wa Chuo
Chuo cha VETA-NKasi,
S.L.P 116.
Namanyere – Nkasi

---

MAELEZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MUDA MREFU KATIKA CHUO CHA VETA NKASI KWA MWAKA 2024

1 Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako ya chuoni:-

i. Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya Tetroni kwa wote na kwa wasichana walio waislamu tu wataruhusiwa kushona nusu gauni na ushungi.

ii. Suruali mbili za bluu kwa wanafunzi ambazo utazikuta chuoni kwa gharama ya Tsh. 40,000/=

iii. Ovakoti moja rangi ya bluu utaikuta chuoni kwa gharama ya Tsh. 25,000/= iv. Fulana (T-shirt) ya VETA utaikuta chuoni kwa gharama ya Tsh 17,000/=

v. Uje na Sweta ya rangi ya bluu iliokolea (dark blue) kama kitambaa kilichoambatanishwa kwenye barua hii)

vi. Kwa wanafunzi wa umeme uje na jozi moja ya viatu vya karakana (Sefety boot)-viatu vyenye chuma mbele pamoja na jozi moja ya viatu vya shule vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi.

vii. Kwa wanafunzi wa Uhazili(Secretatial and Computer) na Ushonaji (Design Sewing and Cloth Tehnology) uje na jozi moja ya viatu vya shule vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi

viii. Kwa wanafunzi wa bweni wanatakiwa waje na
- Shuka mbili za jinja za rangi ya Bluu bahari
- Mto mmoja wa kulalia
- Blanketi
- Chandarua cha rangi nyeupe cha futi 3x6
- Bakuli moja la plastiki
- Sahani moja ya plastiki
- Kijiko kimoja cha chakula
- Kikombe kimoja cha plastiki
- Ndoo ndogo ya plastiki ya lita 10 ya rangi ya Blue kwa ajili ya kuogea pamoja na vifaa vya usafi binafsi.
- Tranka la kutunzia vitu vyako
- Godoro imara lenye kava la upana wa futi 2.5 urefu futi 6 na unene nchi 4 (2.5’x6’x4”)

ix. Wanafunzi wa umeme na ushonaji waje mkebe (mathematical set) na calculator ya kufanyia hesabu calculator (scientific calculator function 991)

x. Wote waje na daftari 10 za Quare 2 au zaidi, kalamu na penseli.

xi. Karatasi ya Ream Paper (zenye ujazo wa 80g/m$^2$)

xii. Wanafunzi wote waje na Pesa ya kupiga picha ya pasipoti Tsh. 3,000/= kwa ajili kuweka kwenye kumbukumbu. Pesa hii utamlipa mpiga picha atakuwepo hapa chuoni siku ya kufungua(Lengo ni kupata picha zenye kipimo na rangi sawa na zenye mfanano kwa ajili ya kuweka kwenye mfumo)

xiii. Wote mnapaswa kuja na kwanja moja na jembe lenye mpini moja.

xiv. Kila mwanafunzi aje na spring file (aina ya RAPID au Maxwel) moja ya rangi ya bluu kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu kwa kila mwanafunzi.

xv. Mwanachuo hatapokelewa chuoni iwapo hatokuja na vifungu vilivyotajwa hapo juu

xvi. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika chuoni na barua yake ya kucahguliwa siku atakapokuja kuanza chuo.

MUHIMU: Ukumbuke kuja na nguo za michezo ambazo ni:-

- Raba za kamba au viatu vya kuchezea mpira wa miguu(six)
- Suruali ya Traki suti ya rangi nyeusi kwa wavulana
- Suruali ya Traki suti ya rangi ya bluu kwa wasichana
- Tshirt ya michezo (ya jezi) ya rangi ya njano kwa wavulana
- Tshirt ya michezo (ya jezi) ya rangi nyekundu kwa wasichana

2 Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyooneshwa kwenye jedwari la malipo ya ada na michanganuo mbalimbali kwa mwaka wa masomo wa 2024

| NA | MAELEZO | BWENI | | | KUTWA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KWA MWAKA MOJA (1) | MUHULA WA KWANZA | MUHULA WA PILI | KWA MWAKA MOJA (1) | MUHULA WA KWANZA | MUHULA WA PILI |
| 1 | SURUALI (2) | 40,000.00 | 40,000.00 | - | 40,000.00 | 40,000.00 | - |
| 2 | OVAKOTI | 25,000.00 | 25,000.00 | - | 25,000.00 | 25,000.00 | - |
| 3 | T-SHIRT | 17,000.00 | 17,000.00 | - | 17,000.00 | 17,000.00 | - |
| 4 | NEMBO YA VETA | 5,000.00 | 5,000.00 | - | 5,000.00 | 5,000.00 | - |
| 5 | BIMA YA AFYA YA TAIFA | 50,400.00 | 50,400.00 | - | 50,400.00 | 50,400.00 | - |
| 6 | PESA YA UKARABATI | 10,000.00 | 10,000.00 | - | 10,000.00 | 10,000.00 | - |
| 7 | KITAMBULISHO | 5,000.00 | 5,000.00 | - | 5,000.00 | 5,000.00 | - |
| 8 | MICHEZO | 10,000.00 | 10,000.00 | - | 10,000.00 | 10,000.00 | - |
| 9 | ADA YA MAFUNZO | 60,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 | 60,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 |
| 10 | ADA YA BWENI | 60,000.00 | 30,000.00 | 30,000.00 | - | - | - |
| | JUMLA | 282,400.00 | 222,400.00 | 60,000.00 | 222,400.00 | 192,400.00 | 30,000.00 |

MUHIMU:-

- MALIPO YA ADA YA MAFUNZO NA ADA YA BWENI YAFANYIKE KUPITIA “CONTROL NUMBER YA ADA” YENYE JINA LA MWANAFUNZI
  - (ADA YA MAFUNZO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NI SHILINGI 60,000/= NA ADA YA MAFUNZO NA BWENI KWA WANAFUNZI WA BWENI 120,000/= KWA KILA MWAKA)

- MALIPO YA SURUALI, OVAKOTI, T-SHIRT, NEMBO YA VETA, BIMA YA AFYA YA TAIFA, PESA YA UKARABATI, KITAMBULISHO NA HELA YA MICHEZO ITALIWA KWENYE
  “CONTROL NUMBER YA MICHANGO” YENYE JINA LA MWANAFUNZI
  - (MALIPO YA MICHANGO YA MWANAFUNZI NI SHILINGI 162,400/=)

“FEDHA IKISHALIPWA HAIRUDISHI. KUWA MAKINI WAKATI WA KULIPA. PESA ZINALIPWA KWA CONTROL NUMBER ZINAZOTOLEWA OFISI YA UHASIBU”

Viambatanisho Vya Maelezo Haya.

1. Barua ya kuchaguliwa kujiunga
2. Fomu ya kuthibitihsa kujiunga na chuo ijazwe na kurudishwa chuoni kabla ya tarehe ya kufungua)
3. Medical Examination Form (Vipimo vifanyike kituo cha afya au Hospitali za Serikali tu)
4. Sheria za chuo

VET MED FORM – 1E

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

MEDICAL EXAMINATION FORM

Date…………………..…..

The medical officer

…………………………………….

…………………………………….

…………………………………….

REQUESTION FOR MEDICAL EXAMINATION:

Name of trainee………………………………………………………

Please Examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently

Work as a/an………………………………………………………………………..

Eyesight………………………………………………………………..………………

Hearing……………………………………………………………………….……………

Asthma……………………………………………………………….…………………

Other serious disease…………………………………………………………..

MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date…………………………………..

Designation ………………………………………………

Signature and Official stamp…………………………………….

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) WANACHUO

Mimi ……………………………………………………………….……… ninakubali nafasi ya mafunzo .Katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

b) MDHAMINI

Mimi……………………………………….………………… ambaye ni mzazi/mlezi/mdamini wa mtajwa Hapo juu nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Sahihi………………………………..…….. Tarehe……………………………………………….

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
VETA NKASI

Simu : 255 - 736117116
Barua-pepe: nkasidvtc@veta.go.tz

Mkuu wa Chuo
Chuo cha VETA-NKasi,
S.L.P 116.
Namanyere – Nkasi

SHERIA ZA CHUO

Ili kufanikisha mafunzo ya awali ya ufundi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zifuatazo

1. MAHUDHURIO
   a. Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya 1:15 asubuhi. Hii ina maana saa 1.15 asubuhi wanafunzi wote wawe chuoni. Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji.
   b. Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, Hospitali, au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kibali cha Mkuu wa chuo.
   c. Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi hata ruhusiwa kufanya mtihani wa kuhitimu mafunzo.
   d. Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuuguwa mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni.
   e. Vyumba au madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.
2. MAVAZI
   a. Sare ya chuo ni suruali ya bluu na shati jeupe mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani isipokuwa siku za jumatano na ijumaa mwanachuo ataruhusiwa kuvaa fulana (t-shirt). Wakati wote shati liwe limechomekewa.
   b. Ovaroli au Overcoat zivaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.
   c. Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au viatu vya wazi (sandals) havirusiwi kuvaliwa chuoni.
   d. Hauruhusiwi kuvaa suruali chini ya makalio (mlegezo) au kurekebisha suruali ibane(iwe model) au kuvaa nguo fupi za kubana uwapo chuoni.
3. USAFI WA MWILI NA MAZINGIRA
   a. Hairusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote kwa kipindi chote cha mafunzo. Hairuhusiwi kutumia vipodozi na manukato yanayotoa harufu kali.
   b. Nywele na ndevu kwa wavulana.
      i. Nywele zikatwe kwa kulingana ziwe fupi na isiwe KIPARA.
      ii. Kufuga ndevu hairuhusiwi kabisa.
      iii. Nywele zisiwekewe dawa ya kuzibadili rangi(Bleach)
   c. Nywele kwa wasichana
      i. Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma(twende kilioni)
      ii. Nywele zisiwekewe dawa ya kuzibadili rangi(Bleach)
   d. Kucha ndefu haziruhusiwi kabisa wala kupakwa rangi.
   e. Hauruhusiwi kutupa taka eneo lolote isipokuwa kwenye vifaa vya kutupia uchafu tu(dustbin)
4. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YOYOTE YULE
   a. Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi aneiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua kali za kisheria zitachukuliwa mara moja
   b. Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au kukirudisha kifaa ulichopoteza.
   c. Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na kilichopo ndani ya chuo. Isipokuwa kwa ruhusa ya mwalimu. Vifaa kama computer / laptop viandikishwe siku ya kuviingiza getini.

   d. Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.
   e. Yoyote atakaebaiinika anatumia vibaya mali ya chuo, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

5. UGOMVI:

Ugomvi,kupigana na kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakaye patikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

6. ULEVI

Iwapo atabainika mwanafunzi amelewa au kuonekana katika sehemu za kileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja dhidi yake.

7. MAPENZI
   a. Uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.
   b. Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo ya wanafunzi au wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

8. MIGOMO

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

9. LUGHA

Lugha itumikayo kuendesha masomo ni kingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kingereza.

10. Hairuhusiwi kubadilisha jina la mwanafunzi mpaka ziwepo sababu na hati maalumu kwa uthibitisho na kibali na kibali cha mkuu wa chuo.
11. MATUMIZI YA SIMU
   a. Hauruhusiwi kuonekana au kuwa na simu wakati wa vipindi kati ya saa 1:30 Asubuhi hadi saa 9:30 Mchana. Endapo utabainika kuwa na simu au kuonekana na simu wakati wa vipindi simu hio itachukuliwa na utakabidhiwa siku ya kumaliza mtihani wako wa mwisho wa kumaliza chuo.
   b. Mwanafunzi wa bweni hauruhusiwi kutumia simu baada ya saa 4:00 Usiku. Endapo utabainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.
   c. Kama kuna dharula ya matumizi ya simu muda wa vipindi, mwanachuo amuone mwalimu wa zamu.

## ONGEZEKO LA SHERIA KWA MWANACHUO WA BWENI

12. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya chuo siku zifuatazo kwa ruhusa ya mkuu wa chuo:
   a. Jumamosi tangu saa 2.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni.
   b. Jumapili na siku za sikukuu tangu saa 2.00 asubuhi hadi 12.00 jioni
   c. Hairuhusiwi kutoka nje ya chuo wakati wowote bila kibali maalumu.
13. Mwanafunzi yeyote anaeruhusiwa nje ya eneo la chuo anapaswa kua na sare ya chuo, kitambulisho cha chuo na atajiandikisha lango kuu. Mwanafunzi atakaye kiuka masharti tajwa hapo juu, atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang’anywa nafasi ya bwenini au kufukuzwa chuoni.
14. Mwanafunzi atakaye patikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo na kupoteza sifa za kuwa bweni au kupoteza nafasi ya masomo kulingana na ukubwa wa kosa.
15. Hairuhusiwi kupika chakula bwenini au eneo la chuo atakae kiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.
16. Ni marufuku mwanachuo wa kiume kutembelea bweni la wanafunzi wa kike na mwanachuo wa kike kutembelea bweni la kiume.

17. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.
18. Hairuhusiwi kupokea au kuingiza chakula chochote ndani ya chuo kutoka nje ya chuo isipokuwa kwa kibali maalumu toka kwa mwalimu wa zamu.
19. Taa za madarasani na mabweni zizimwe saa 4:00 za usiku.
20. Hairuhusiwi kumkaribisha au kumlaza mgeni bwenini, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.
    a. Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea wanachuo kila Jumamosi kuanza saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.
    b. Kila jumapili na siku za sikuu kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni.
21. Hairuhusiwi kulala nje ya chuo. Iwapo itatokea ruhusa itatilewa na ofisi ya mkuu wa chuo.
22. Mwanachuo anaeishi bweni hakikisha unatandika kitanda chako muda wote, na kuhakikisha choo mnachotumia ni safi na kiwe hakinuki na pia kina maji ya kutosha muda wote.